Huduma ya Hifadhi ya ukimbizi inahusika na maswala ya ulinzi wa kimataifa. Kama wewe ni mgeni na umekimbia nchi yako kwa sababu ulikuwa ba matatizo makubwa, hatari kubwa, una haki ya kuwasilisha ombi la ulinzi wa kimataifa.

Tunakufahamisha (kukujukisha) kwamba Huduma ya Hifadhi ya ukimbizi haichukui maombi ya ulinzi wa kimataifa kama tayari umeisha wasilisha ombi la ulinzi wa kimataifa kwenye polisi ambao bado haujapata majibu yake ama unayo pinki kadi.

Inapashwa uje mwenyewe kwenye offisi zetu za huduma ya hifadhi ya ukimbizi za mikoa kwa kutoa , kuleta ombi lako. Ma offisi za mikoa zinapatikana Athina, Thessaloniki, Rodo,Orestiada na Alexandroupoli.Kuwasilisha maombi ni kwa bure. Kwa iyo unaweza kuja kwenye huduma zetu na mwanasheria (loya,lawyer) ambae ni wewe mweyewe utakae mlipa. Kutakuwepo pia mkalimani( mtafsiri, interpreter) ambae atakusaidia kwa kuwasilisha ombi lako. Kama unayo cheti ambazo zinazibitisha kitambulisho chako, kama vile passpoti, ao cheti chochote , itapashwa uzilete ukujapo. Wakati wa kuwasilisha ombi lako, utapigwa picha na kuchukuliwa vidole.Unaweza kuwasilisha ombi pia kwa ajili ya familia yako ambao ni lazima wawe pamoja na wewe wakati utakapo kuja kwenye Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi. Kama upo chini ya miaka 14 nai hausindikizui na mtu mkubwa ambae anaye ajibika wangalifu, utunzo wako, serikali ya ugiriki itachukua majukumo ya matunzo, wangalifu wako.Kama umeisha wasilisha ombi lako la ulinzi wa kimataifa tunakujulisha ,kufahamisha ya kwamba ni muhimu sana uwe kila mara na kadi (cheti) ya muombaji wa ulinzi wa kimataifa , na uje kwenye huduma (offisi) zetu kwa ajili ya kuongeza mda wake siku inayofata baada ya kumalizika kwa cheti iyo.

Kama ukibadili namba ya simu ao anwani, unalazimishwa ujulishe kwa haraka Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi.

**HABARI ZA MSINGI KWA WAOMBAJI WA ULINZI WA KIMATAIFA NCHINI UGIRIKI.**

Mwombaji wa ulinzi wa kimataifa ni mgeni au mtu bila uraiya,ambaye anashuhudia kwa mdomo au kwa maandiko kwenye mamlaka yoyote yaki giriki ( serikali ya kigiriki) kwamba anaomba hifadhi ya ukimbizi au anaomba asi fukuzwe nchini kwa sababu anaogopa harakati kwa sababu ya rangi, dini, kabila, ushiriki kwenye kikundi fulani cha kijamii au imani kisiasa, au kuna uwezekano wa mateso makubwa, hatari kupata madhara makubwa nchi yake ya asili ao makazi yake ya zamani, au kwa sababu kuna hatari ya adhabu ya kifo au kunyongwa, utesaji au unyama au uadilifu wa maisha yake kwa sababu ya vita ya kimataifa ao vita vya kiraia ( vita vya wenyewe kwa wenyewe).
Mwombaji wa ulinzi wa kimataifa ni pia mgeni ambaye ameingia nchini ugiriki kutokana na kanuni ya <<Dublino II[1]>>

**Ombi la ulinzi wa kimataifa: Wapi na Vipi utaliomba**

• Mamlaka ambayo inausika na ombi lako ni Ofisi ya Hifadhi ya Ukimbizi za Mikoa na vikundi vya kazi vya Offisi ya Hifadhi ya Ukimbizi za Mikoa.

**MAKINI**
Tunawajulisha ya kwamba Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi haina wajibiki wa uchukuzi wa ombi lenu: a) Kama umeisha wasilisha tayari ombi la Hifadhi ya Ulinzi wa Kimataifa kwenye polisi ambayo bado haujapewe majibu, b) Kama unayo cheti cha mwombaji wa hifadhi ya ukimbizi (pinki kadi)
Tunawajulisha pia kwa kila kesi mutachukuliwa vidole ili Hifadhi ya Uduma ya Ukimbizi ipate kutizama kama bado mumeisha wasilisha tayari ombi la hifadhi la kimataifa, na kwa iyo itatizamwa moja kwa moja kama munasubiri majibu kutokana na ombi lenu.

• Kama wewe ni mfungwa au unaishi kwenye vituo vya Mapokezi ya Mwanzo, huduma zenye mamlaka ya ufungwa ao ya mapokezi ya mwanzo yaani kituo cha polisi ambapo umefungwa ao kituo cha mapokezi ya mwanzo ambapo uanishi, wanatakiwa kujulisha Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi kuhusu nia yako ya kuomba ulinzi wa kimataifa.

• Unatakiwa kuomba (kuwasilisha ombi) ulinzi wa kimataifa wenyewe kibinafsi, kwa mdomo au kwa maandiko. Unaweza kuomba, kuwasilisha ombi pia kwa ajili ya familia yako kama wako na wewe Ugiriki na kama wakitaka.

• Wakati unawasilisha ombi, wakati unomba ulinzi wa kimataifa, na kama hauelewani kilugha na mfanyakazi (offisa) wa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi , ujuwe wa kwamba kutakuwepo mkalimani (mtafsiri, interpreter) kwa kukusaidia.

• Wakati unawasilisha ombi lako unatakiwa kujibu kwa ukamalifu kwa maswala ya mfanyakazi (offisa), yaani majibu yawe kamili na ya ukweli. Kama ukitoa maelezo, habari, dhati za uongo au madai ya uongo, ujue kwamba yataathiri kwa uamuzi wa ombi lako.

• Kama wewe ni mdogo, yani upo chini ya miaka 18 na hujasindikizwa na mtu mkubwa au mtu mwenye dhamani yako, kulingana na sheria ya Kigiriki ao mazoezi, serikali ao offisa wenye mamlaka, wanatakiwa watoe habari haraka kwa Wakili mwenye uwezo. Wakili atakupa mwakilishi (kamishani) ambaye atakua na wajibu wako na kutetea maslahi yako.Kama upo chini ya miaka 14 ombi lako la ulinzi wa kimataifa inatakiwa iwasilishwe na mwakilishi utakae pewa. Kama wewe umepitisha miaka 14 unaweza kuomba mwenyewe. Serikali (offisa yenye mamlaka) itategemea ulinzi wako na sehemu ambayo utakayoishi iwe sehemu nzuri kwa watoto wadogo.

• Wakati unaomba ulinzi wa kimataifa (wakati unawakilisha ombi lako), utapigwa picha na kuchukuliwa vidole, pamoja na familia yako ambao wako juu ya miaka 14. Vidole ivyo

---

Inchi zinafungamana na kanuni ya Dublino II ni: Austria, Bulgaria, Chekia, Denmark, Estonia, Finland, Holland, Hungaria, Italia, Irlandia, Islandia, Cyprus, Letonia, Liechtenstein, Lithuania, Luxemburg, Malta, Norway, Poland, Romania, Slovakia, Slovenia, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Ujeremani, Ureno, Uswisi, Uwigereza.

vitaingizwa kwenye Msingi (Data) Kuu ya Ulaya EURODAC na kama umeisha omba ulinzi wakimataifa inchi ingine ya Ulaya inayo tumia sheria (kanuni) <<Dublino II >> utarudishwa (Utapelekwa) ili ombi lako litizamwe uko.

- Lazima utoe vyeti vya usafiri (passpoti) ao cheti (hati) chochote unacho na ambacho kinahusiana na uchunguzi wa ombi lako na kuthibitisha kitambulisho chako na cha watu wa familia yako, nchi yako na sehemu ganu umetokea, pia hali yako ya kifamilia.
- Ukisha wakilisha ombi, unaweza kufanyiziwa utafiti wa mwili au utafiti wa vitu utakua navyo.
- Huduma ya Hifadhi wa Ukimbizi itakupa tarehe ya mahojiano na utapewa cheti cha muombaji wa ulinzi wakimataifa (pinki kadi) ambayo inaweza kuwa na muda wa miezi 6. Cheti icho unatakiwa uwenacho kila mara.
- Wakati unapo wasilisha ombi lako, unapo peleka ombi lako, mamlaka ( offisa wa serikali) wana wajibu kukufahamisha, kukupa maelezo kwa lugha ambayo unaelewa , kutokana na utaratibu,haki zako na majukumu yako kama muombajni wa ulinzi wa kimataifa, na kwa muda uliyo kutokana na muda wa utaratibu wa uchunguzi wa ombi lako.
- Kama weye ni mtu ambae umeathirika, kusumbuliwa na mateso, kubakwa au mateso mengine mbali mbali, unatakiwa ujuulishe mamlaka (offisa wa serikali) ili wakusaidie.
- Unaweza omba pia uwasiliana na Offisi ya Umoja mataifa kwa Wakimbizi (UNHCR) au shirika, kikundi ambayo inatoa msaada wa kisheria, matibabu na ushauri wa nasaha.
- Kwenye muda wa utaratibu wa uchunguzi una haki ya kuomba usaidizi kutoka kwa loya (mwanasheria) au mshauri yoyote utaechangua mwenyewe (bila upatanishi wa Hifadhi ya Ukimbizi). Malipo ya loya au mshauri yatakua juu yako wewe kibinafsi (ni wewe ambae utakao mlipa loya ao mshauri).
- Kama ukitaka, unaweza pewa muda wakujitaharisha vizuri kuhusu mahojiano (intavyu) kwa ajili ya kupata msaada kutoka kwa loya au mshauri yeyote ili akusaidie katika utaratibu uyo.
- Kama wewe ni mwanamke unaweza omba intavyu, mahojiano yako yafanyikwe na mfanyakazi (offisa) wa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi wa kike pia mkalimani (mtafsiri ) wa kike, kama wakiwepo.
- Kwa kila kesi unaweza omba mahojiano, intavyu na utasfiri ifanyikwe na mfanyakazi wa hali ambao unayo taka, kama upo mwanaume , anaweza kuwa na kiume, na kama upo mwanamke anaweza kuwa wa kike, kama kuna mambo muhimu kuhusu swala ilo. Ombi lako litatizamiwa na Huduma.
- Kama we ni mtoto mdogo alafu uko mwenyewe majukumu ya intavyu, mahojiano yako atafatilia mwakilishi wako.Mwakilishi wako ataitwa na anaweza kuwa na wewe katika inatvyu , mahojiano yako.Serikali, (ofisa wenye huduma) wanaweza kukuchunguza kwa kutumia dokta ili wa jue miaka yako.Ili waweze kufanya uchunguzi huo wa hospitali, ni lazima mjulishwe wewe na mwakilishi wako na munatakiwa mkubali ili yaweze kufanyika.

**Kujiuzuru na kurudisha uombaji wa Ulinzi wa Kimataifa**

- Unaweza kujiuzuru kwenye ombi lako wakati wowote utakapo mwenyewe. Unatakiwa kwenda mwenyewe kwenye Offisi ya Hifadhi ya Ukimbizi za Mikoa na kijiuzuru kwa maandiko. Na kama ukijuuzuru huduma haita chunguza tena ombi lako na unatakiwa kuondokea nchini kwasababu hauna cheti chochote kinacho kuruhusu kuhishi nchini.
- Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi inaweza kufikiria ya kwamba hauna nia ya kuendelesha uchunguzi wa ombi lako (thabiti ya uondoaji wa maombi) na kuweza kusimamisha ombi lako:

a) Kama ukikataa kutoa taarifa ya muhumu zaidi kwa ajili ya ombi lako ambayo imeombwa na Serikali (Offisa mwenye huduma) au,
b) Kama haukwenda kwenye intavyu, mahojiano au,
c) Kama umekimbia sehemu unayoshikwa, uliyofungwa au

d) Kama umeshindwa kushika majukumu ambayo polisi aliyo kupa badala ya kukufungwa au,
e) Kama ukiondoka sehemu uliopewa ya kuhishi na Serikali bila kuwataarifu, au
f) Kama ukiondoka nchini bila kuomba usaidizi kutoka Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi, au
g) Kama hujalulisha kwa haraka Huduma ya Hifadhi ya Ulinzi kuhusu umebadilishaji wa anwani yako na ginsi yakuwasiliana (namba ya simu),
h) Kama ujawasiliana na Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi wanapokuitaji,
i) Kama haujaenda kuongeza muda cheti chako (pink kadi) ukichelewa, siku inayofata kabla haijaisha. Na kama Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi inasimamisha uchunguzi wa ombi lako, unayo haki ya kuomba waendelee kuchunguza ombi lako.Unatakiwa wende kwenye Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi ili uwaeleweshe sababu ambayo Huduma haipaswi kuchukuliwa
kwamba huna nia waendelee kuchunguza ombi lako.Huduma ndio itakao hamua.

**Utaratibu wa kufatilia uombaji wa ulinzi wa kimataifa**

- Siku ambayo utakayo pewa na Huduma kwa ajili ya mahojiano, utatoa mahojiano iyo kwa mfanyakazi wa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi.Unatakiwa ujibu kwa ukweli zaidi kwenye maswali yake, kusema matukio ya ukweli tu kwa kila kitu kilichotokea na usifiche kitu chochote ambacho kinahusika na ombi lako.Na kama ukitoa taarifa za uongoau madai za uongo itaathiri wenda vibaya uhamuzi kwenye uchunguzi wa ombi.
- Mfanyakazi wa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi atakuuliza kwenye mahojiano (intavyu) yako kuhusu habari, maelezo ambazo zipo kwenye ombi lako, za kitambulisho chako, vipi (namna gani) umeingia ugiriki, sababu zilizo kufanya uondoke kwenye nchi yako au nchi ambayo ulikua unaishi, kama wewe hauna urahiya wa inchi lolote, na pia sababu ambazo hauwezi kurudi au hautaki kurudi katika nchi hiyo.Kwenye mahojiano ( intavyu) yako unaweza kuongeza habari, maelezo yeyote unaona muhimu na inaweza kukusaidia.
- Kama, ni kwa sababu ya lugha hauwezi kuelewana na mfanyakazi wa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi kwenye mahojiano (intavyu) atakuwepo mkalimani, mtasfiri wa kukusaidia.
- Kwenye mahojiano (intavyu, interview) unaweza kwenda na mwanasheria (loya) au mshauri mwengine (mwanasheria, dokta, mwanasaikolojia, au mshauri wa jamii (sosial woka).
- Kila utakachosema kwenye mahojiano kitakuwa siri.
- Mahojiano inaweza kurikodiwa.Mwisho wa mahojiano mfanyakazi wa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi ataandika ripoti ikiwa pamoja na madai ya vitu ulivyosema katika muda wa mahojiano yenu na kila habari, maelezo muhimu ya mahojiano.Kama mahojiano yako haita rikodiwa,basi mfanyakazi ataandika nakala(jaribio)ambayo atakayo kuwa na maswala na majibu yote ya mahojiano yako. Kwa iyo unatakiwa kucheki nakala ya jaribio kwa msaada wa mtafsiri wa lugha au unaweza kuomba marekibisho baadaye unaweza kusaini. Unaweza wakati wote utakapo kuchukua kopi ya nakala hiyo au ripoti ya mahojiano ambayo iliyorikodiwa.
- Baada ya mahojiano (intavyu) Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi itaamua kukupa hadhi ya ukimbizi (yaani kukubaliwa wewe kuwa mkimbizi) ama kuwa mwenye hifadhi ya ulinzi au kukataa ombi lako.
- Baada ya kutoa uwamuzi kuhusu ombi lako Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi itakujulisha ili uje ukachukue uwamuzi uyo.Watakujulisha kutokana na uwezo wa mawasiliano uliyo toa ao kwa simu, aokwa barua, ao kwa fax, ao kwa email.
- Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi inatakiwa ikujulishe uwamuzi kwa kutumia mtafsiri kwa lugha unayoelewa vizuri.
- Na kama bado haujapokea uwamuzi na haujaenda kuongeza muda wa cheti chako (yaani ku rinyu pink kadi yako) kabla haijaisha, ukichelewa sana, siku ifautayo tarehe ya

kumalizika kwake, basi Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi itafikiri kama umeisha pokea uwamuzi siku walikutumia.

**Majukumu ya uombaji wa ulinzi wakimataifa**
Kama muombaji wa ulinzi wa kimataifa inchini ugiriki, unayo wajibu:

- Unatakiwa ubaki (kukaa) ugiriki hadi wamalize kucheki (kuchunguza) ombi lako.
- Wa kushirikiane na Serikali ya ugiriki kwa kitu chochote kinachohusu ombi lako na kuthibitisha kitambulisho chako.
- Wa kwenda mwenyewe kwenye Huduma wa Hifadhi ya Ukimbizi kwa kuongeza muda wa cheti chako (pink kadi yako) siku ifuatayo kabla yakumalizika kwa cheti iyo.
- Wa kutoa taarifa haraka kwenye Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi ya kwamba umebadilisha anwani yako na ginsi yakuwasiliana nawe (namba ya simu), pia na wakati unapo zibadili.Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi itatuma kwenye anwani uliyo wapa makaratasi, dokimenti, vyeti ambavyo vinayohusika na ombi lako.
- Wa kuhueshimu mipango ambayo utakayo pewa kuhusu utaratibu wa uchunguzi wa ombi lako.
- Kujulisha hali yako ya kipesa kamili ukiwa unapata msaada kutoka kwenye Serikali.
- Kuheshimu majukumu watakayo kutolea ikiwa unaishi kwenye kambi ya ugeni ao nafasi yeyote.

**Haki ya waombaji ulinzi wa Kimataifa**
Kama mwombaji wa hifadhi ulinzi wa kimataifa ugiriki:

- Inakatazwa ufukuzwe nchini hadi walimalize kucheki (kuchunguza) ombi lako.
- Unaweza kutembea uhuru nchini, labda kama kwenye cheti (pinki kadi) yako imeandikwa sehemu (nafasi) maalumu za nchi ambapo unaweza, unapashwa kutembea.
- Kama hauna sehemu (nafasi) ya kuishi unaweza kushughulikiwa, kupewa nafasi ya kulala kwenye Vituo vya Ukarimu (vituo vya kuifadhi wageni) au sehemu nyengine.
- Una haki yakufanya chini ya masharti yaliyowekwa na sharia ya Ugiriki.
- Una haki sawa sawa za usalama na majukumu, kama mfanyakazi, kama wanainchi wa ugiriki.
- Una matibabu za dawa kwa bure na matibabu ya hospitali kwa bure.
- Watoto wako wanayo nafasi -na wewe kama mwenyewe kama ni mdogo, kwenye elimu kwa bure (bila kulipa).
- Una nafasi ya kupata mafunzo ya ufundi.
- Kama wewe ni mlemavu yaani mtu kilema kwa 67% na juu, una haki upate malipo (misaada) ya ulemavu, ya vilema, ikiwepo haitakuwepo uwezo wa kuishi kwenye kituo cha ukarimu.
- Kama mwombaji wa hifadhi ya kimataifa hauwezi kusafiri inje ya ugiriki.
- Kama mwombaji hauwezi kuleta familia yako kutoka nchi unayo tokea (inchi yako).

**Haki ya rufaa (apili) na Uchunguzi kwa kamiti (digri) la pili**

- Kama ombi lako imekataliwa,au umekukubalia hadhi ya Hifadhi ya Ulinzi na unafikiri ya kwamba unatakiwa upewe hadhi ya mkimbizi (yaani unafikiri kama unatakiwa kukubaliwa kuwa mkimbizi) ,una haki yapeleka rufaa (apili) mbele ya kamati ya Rufaa (kamati inayo tizama rufaa zilizopelekwa).
- Unatakiwa upeleke rufaa iyo kwenye Ofisi ya Hifadhi ya Ukimbizi za Mikoa ao vikundi vya ofisi ya Hifadhi ya Ukimbizi za Mikoa iliyo kupa uwamuzi kwenye tarehe ya mwisho (muda) iloandikwa kwenye uwamuzi uliyopewa.
- Muda huo (tarehe ya mwisho) inaanza siku ifautayo baada ya siku uliyopokea uwamuzi. Lakini kama haujapokea uwamuzi na haujaenda kuongeza muda wa cheti lako (kurinyu pink kadi yako) uchelewapo siku ifuatalo baada ya kuisha kwake, muda (tarehe ya

mwisho) itaanza siku hiyo (yaani siku ifuatayo umalizikaji wa cheti, siku ifuatayo baada yakupita raheye ya pinki kadi yako).

• Kamati ya ma Rufaa inaweza kufikiria ya kwamba hauna nia ya kuendelesha uchunguzi wa ombi lako (thabiti ya uondoaji wa maombi) na kuweza kusimamisha ombi lako:

a) Kama ukikataa kutoa taarifa ya muhumu zaidi kwa ajili ya ombi lako ambayo imeombwa na Serikali (Offisa mwenye huduma) au,

b) Kama haukwenda kwenye intavyu, mahojiano au,

c) Kama umekimbia sehemu unayoshikwa, uliyofungwa au

d) Kama umeshindwa kushika majukumu ambayo polisi aliyo kupa badala ya kukufungwa au,

e) Kama ukiondoka sehemu uliopewa ya kuhishi na Serikali bila kuwataarifu, au

f) Kama ukiondoka nchini bila kuomba usaidizi kutoka Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi, au

g) Kama hujalulisha kwa haraka Huduma ya Hifadhi ya Ulinzi kuhusu umebadilishaji wa anwani yako na ginsi yakuwasiliana (namba ya simu),

h) Kama ujawasiliana na Mamlaka (kikao) ya Rufaa wanapokuitaji ao,

i) Kama haujaenda kuongeza muda wa cheti chako (pink kadi) ukichelewa, siku inayofata kabla haijaisha.

• Ikiwapo Kamati ya Rufaa (yaani kamati inayo tizama rufaa zilizopelekwa) inaamua kukuita kwenye mahojiano (intavyu) utajulishwa siku 5 (siku ambazo zinazofanywa kazi) kabla ya siku ya mahojiano (intavyu). Una haki ya kwenda kwenye Kamati ya Rufaa na loya wako au na mshauri mwengine. Na hatakama hakuenda kwenye Kamati ya Rufaa (kamati inayo tizama rufaa zilizopelekwa), rufaa (apili) yako itachekiwa, kuchunguzwa kwa kawaida.

• Kamati ya ukimbizi itaamua kama itakupa radhi ya ukimbizi (yaani kukubaliwa kama mkimbizi) au utapewa radhi ya Hifadhi ya ulinzi au itakataa rufaa lako.

• Kwa kuchukua, kupokea uamuzi kutoka ya Rufaa (kamati inayo tizama rufaa zilizopelekwa) taratibu ni sawa sawa na yale wa kupewa uamuzi wa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi.

• Kama ombi lako imekataliwa, au umekukubalia hadhi ya Hifadhi ya Ulinzi, na unafikiri ya kwamba unatakiwa kupewa hadhi ya mkimbizi (yaani unafikiri kama unatakiwa kukubaliwa kuwa mkimbizi), unaweza kufanya ombi la kukataa uamuzi kutoka mamlaka ya Mahakama.

**Kufungwa kwa waombaji ulinzi wa kimataifa**

Lazima ujue ya kwamba:

• Mwombaji wa ulinzi wa kimataifa hafugwi kwa sababu tu ameingia na anaishi kinyuma ya sheria inchini.

• Kama uliomba, uliwasilisha ombi la ulinzi wa kimataifa na umefungwa kwa sababu umefanya kosa (jinai) utabaki chini ya ulinzi wa sheria yaani kufungwa.

• Kama uliomba, uliwasilisha ombi la ulinzi wa kimataifa na wewe bado upo mfungwa kwasababu umeingia nchini kinyume cha sheria au kama bado haijatolewa uwamuzi wa kuondoshwa kwako nchini , inawezekana polisi akiamua kama kwa kesi lako ni lazima, ubaki chini ya ulinzi wa sheria( mfungwa):

**a)** ili watizame kama ni kweli uliyo toa habari, maelezo kuhusu kitambulisho chako au mahali ambayo unayotokea,au

**b)** kwa sababu unafikiriwa kuwa hatari wa usalama ya taifa au hatari ya umma au

**c)** kwa sababu kukaa kwako chini ya ulinzi ya sharia (kufungwa kwako) inachukuliwa muhimu ili wapate kuchunguza kwa haraka ombi lako (na ile ambao uliyo wasilisha, uliyo omba kwenye huduma ya mapokenzi ya kwanza ya Mkoa). Kwenye tukio kama ilo, serikali, huduma wenye mamlaka wa uchunguzi, wanatakiwa kuchukua hatua muhimu ili iweze kuchunguzwa kwa haraka ombi lako

- Polisi ya ugiriki inaweza kuamua kufungwa kwako, kubaki chini ya ulinzi wa sheria hata kama hauko mfugwa, katika kesi ya pekee na kama unafikiriwa kuwa hatari wa usalama ya taifa au hatari ya umma, kwa iyo ni bora ubaki chini ya ulinzi wa serikali yaani ufungwe.
- Kifungo chako kinaweza kuwa cha miezi 3 hadi miezi 18 kutakona na kesi ya kifungo chako.
- Kuhusu Kifungo chako anaamua Mkuu wa polisi ambayo anapashwa kufasiria kwa kirefu kwenye uamuzi wake, kwanini kahamua kifungo chako yaani kubaki kwako chini ya ulinzi wa sheria.
- Katika uamuzi huo wakufungwa, wa kubali chini ya ulinzi wa sheria una haki ya kupinga mbele ya Mkubwa au kwa hakimu mahakama ya kwanza mwenye mamlaka wa tawala Mkoani ambapo, yaani sehemu (Mkoa) ambayo umefungwa.
- Kama wewe ni mfugwa au unahishi kambini cheti cha muombaji wa ulinzi wakimataifa (pinki kadi) inatakiwa upewe baada ya kuachiwa au ukisha toka kambini na unatakiwa ndani ya siku 10 uende kwenye Ofisi ya hifadhi ya Ukimbizi ya Mkoa iliyo karibu ili utoe habari, ginsi ya kuweza kuwasiliana na wewe (kama vile numba ya simu na anwani yako).

**Habari muhimu wakati unapo wasilisha ombi lako (unapo omba) la Ulinzi wa Kimataifa**

- **Kama ikitokea habari mya za muhimu** ama baada ya wewe kukataliwa rufaa ( apili) yako kwenye Kamati ya Rufaa yaani Kamati iyo ya kutizama ma rufaa, au baada ya kukataliwa ombi lako kutoka kwa Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi na baada ya mwisho wa muda ambao uliyo pewa kumalizika, kupita ambapo ulitakiwa kupeleka ombi lako la rufaa, unaweza kuwasilisha ombi mpya ,kuomba upya (baadae)
- Ni lazima kuwasilisha ombi lako la baadaye (kuomba baadae) kwenye Ofisi ya Hifadhi ya Ukimbizi ya Mkoa ama kwenye vikundi vya kazi vya Ofisi ya Hifadhi ya Ukimbizi wa Mikoa. Unatakiwa upeleke, uwe na uamuzi ambao haikukubaliwa ombi lako la kwanza (yaani uamuzi ambao walikataa ombi lako la kwanza) na kwa kupeleka kwa kuandika (yaani kwa maandiko) habari mpya muhimu zilizotokea. Baada ya kuwasilisha ombi lako la baadae, hautapewa cheti cha mwombaji hifadhi ya kimataifa.
- Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi itachunguza habari mpya, maelezo mapya uliyowasilisha, na itahamua kama ni muhimu kwa ajili ya ombi la ulinzi wa kimataifa.
- Kama Huduma ikikataa ombi lako la baadae unaweza kufanya rufaa (apili) kwenye kamati ya ma rufaa (kamati inayo tizama rufaa zilizopelekwa) ndani ya muda wa siku 15 (15 days). Muda huo unaanza siku ifuatao kuanzia siku uliyo pokea uwamuzi.

Tunataka kuwafahamisha ya kwamba, inakatazwa kuingia kwenye maeneo ya Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi: Silaa, Vitu vikali, ao vitu vyovyote ambavyo vinaweza kutumiwa kwa kuleta jeraha,vifaa vya kuripuka ao vya kuwaka, dutu za kemikali ao za sumu.
Pia, inakatazwa kuingia kwa watu wanoa kuwa na mizigo ao mifuko, isipokuwa tu briefcase, na mifuko midogo za mikononi.
Matumizi ya simu ya mkononi (mobile phone) itaruhusiwa tu kwenye maeneo za inje ya Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi, ila haitaruhusiwa upikaji wowote wa picha ao video ndani na inje ya maeneo ya Huduma ya Hifadhi ya Ukimbizi.

**KANUNI "DUBLIN II"**

Wakati unawakilisha ombi la hifadhi ya kimataifa, utakuchukuliwa vidole, pamoja na familia yako ambao wako juu ya miaka 14. Vidole ivyo vitaingizwa kwenye Msingi (Data) Kuu ya Ulaya EURODAC ambao inataka utekelezaji wa Kanuni ya "Dublin II".
Kanuni ya <<Dublin II>> inaamua ni inchi gani za ulaya, inayofungamana nayo, ina wajibu wa kuchunguza ombi lako:

Inchi zinafungamana na kanuni ya Dublin II ni: Austria, Bulgaria, Chekia, Denmark, Estonia, Finland, Holland, Hungaria, Italia, Irlandia, Islandia, Cyprus, Letonia, Liechtenstein, Lithuania, Luxemburg, Malta, Norway, Poland, Romania, Slovakia, Slovenia, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Ujeremani, Ureno, Uswisi, Uwigereza.

- Na kama wewe ni mtoto mdogo bila mtu (memba) wa kukusindikiza na kuna mtu wa familia yako ambae anaishi kihalali, kisheria katika nchi yoyote ya ulaya, ni nchi iyo ina wajibu wa kuchunguza ombi lako.

Kama memba wa familia ni kwamba familia ilikuwepo tangu zamani inchi ya asili na sasa ivi memba anapatikana kwenye inchi moja za apo juu ni: mke ao mume ama mtu anaishi na mwengine kihalali (mtu uyu hakubaliwe kama memba wa familia kwenye inchi zote), watoto wadogo wasiolewa ama kuowa. Kama upo motto mdogo asiye owa ama kuolewa, memba wa familia ni pia baba, mama yako ao mlizi wako.

- Na kama wewe ni mtoto mdogo bila mtu wa kukusindikiza na kuna mtu (memba) wa familia yako asiye ishi kihalali kwenye inchi moja za "Dublin II", Ugiriki ndio itachunguza ombi lako.
- Na kama kuna mtu katika familia ameisha tambuliwa kama mkimbizi au yupo mwombaji wa hifadhi ya ukimbizi katika nchi yoyote ya " Dublin II", kama unataka ni wajibu ya inchi iyo kuchunguza ombi lako.
- Kama unayo kibali cha kuishi ( residence permit), inchi inayo wajibu wa kutizama ombi lako ni inchi ya "Dublin II" iliyo toa kibali icho cha kuishi (residence permit), ata kama ikiwa imekwisha muda kabla ya miaka 2
- Kama unayo ruhusa ya kuingia nchini (viza) , inchi inayo wajibu wa kuchunguza ombi lako ni nchi ya "Dublin II" ilio toa ruhusa ya kuingia (viza ) ata kama itakuwa imekwisha muda kabla ya miezi 6.
- Kama unayo vibali vya kuishi juu ya kimoja ama viza, ni inchi gani ya "Dublin II" inawajibu wa kuchunguza ombi lako, itatokana na muda na tarehe ya kumalizika vibali ivyo vya kuishi ao viza.
- Kama umeingia kwenye inchi moja ya "Dublin II" kinyume ya sheria, ukitokea inchi isiyo kuwa ya "Dublin II" inayo wajibu ya kuchunguza ombi lako ni inchi iyo. Wajibu huyo haupiti miezi 12 baada ya kuingia kwako kinyume.
- Pia, kwa kesi ambao kabla ya kuwasilisha ombi lako, uliwayi kuishi inchi ingine ya "Dublin II" kwa muda wa miaka 5 zinazofuatana, wajibu ni wa inchi iyo ambayo ulikuwa umeishi.
- Kama umeingia kihalali, kisheria kwenye moja ya "Dublin II" ambayo hauitaji viza, inchi iyo inawajibu wa kuchunguza ombi lako.
- Kama umewasilisha ombi kwenye eneo la kimataifa yoyote ya ndege ya inchi yeyote ya "Dublin II", ni inchi iyo inayo wajibu wa kuchunguza ombi lako.
- Kama tayari umeisha wasilisha ombi lako kwenye inchi lingine la "Dublin II", inchi iyo inawajibu wa kuchunguza ombi lako.

- Inchi yeyote ya “Dublin II” inaweza kukubali kuchunguza ombi lako kwa sababu za kibinadamu.
- Kama ikiwa kesi lako haiwasiliane kwa vyovyote na hizo kesi za hapo juu basi inchi inayo wajibu wa kuchunguza ombi lako ni Ugiriki.
- Kulinganisha na na kesi za hapo juu, kama nchi nyingine ya “Dublin II” ina wajibu wa kuchunguza ombi lako na inakubali kulichunguza, basi ombi lako la Ugiriki litakataliwa kama lisivyo wezekana na utapelekwa nchi nyengine kwa kanuni ndani ya miezi 6 kuanzia tarehe ilyo kubali kuchunguza ombi lako.
- Dhidi ya uwamuzi huo, una haki ya kuomba uchunguzi upya wa kesi lako (kupeleka rufaa, apeli) kwenye Mamlaka ya Rufaa kwenye muda ambao unaandikwa kwenye uamuzi uliyopokea.

Kwa kusudia utekelezaji wa sheria za vyote vilivyo elekezwa hapo juu, wakati unapowasilisha ombi la ulinzi kimataifa unatakiwa kujulisha mamlaka wanayo husika kuhusu vitu vifuatavyo:
1) Kama unayo viza ya inchi yeyote ya “Dublin II”,
2) Kama una kibali cha kuishi cha inchi yeyote ya “Dublin II”,
3) Kama umeinga kinyume cha sheria Ugiriki kwa kupitia, kutumia inchi nyingine ya “Dublin II”,
4) Kama uliishi kinyume ya sheria kwenye inchi nyingine ya “Dublin II”,
5) Kama kuna watu wa familia yako anaishi kwenye inchi nyingine ya “Dublin II”.

Unatakiwa utoe habari, maelezo muhimu na kuthibitisha ushahidi, cheti ulicho kuwa nazo. (kama vile vibali vyako vya kuishi na vya familia yako,hadhi ya ndoa au vyeti vyengine,viza,makaratasi ambayo yanaonyesha mahali uwepo kwenye nchi nyingine,au kama vile tiketi ya usafari,au risiti ya hoteli na vingine vingi).

# MAMBO 10 AMBAZO MUNAPASHWA KUZIJUA

1) Lazima uwasilishe (peleke) ombi ya ulinzi wa kimataifa mwenye (peke yako), kwa mdomo ao kwa maandiko. Unaweza pia kuwalisilisha ombi kwa ajili ya familia yako ambao wapo pamoja nawe.

2) Wakati unapokuja kwenye Huduma ya Hifadhi ya ukimbizi, kama hauwezi kuelewana na mfanyakazi (offisa) wao, atakusaidia mkalimani (mfasiri).

3) Wakati unapowasilisha ombi lako, ni lazima ijibu kwa ukweli ku maulizo za mfanyakazi (offisa). Ikiwa umesema uwongo ao madai ya uwongo, itaathiri wenda vibaya (negative) uhamuzi wa ombi lako.

4) Wakati unawasilisha ombi lako, utapigwa picha na utachukuliwa vidole pia na familia yako ambao iko na miaka zaidi ya 14.

5) Lazima utoe passpoti ao cheti (hati) yeyote unayo na ambao inaasiliana na kesi lako ili ithibitishwe kitambulisho chako na cha familia yako, nchi umetoka, pia hadhi ya ndoa yako.(kama umeowa, olewa ao hapana).

6) Lazima ushirikiane na serikali ya ugiriki kwa kila kesi kinacho husu ombi lako na kuthibitisha kitambukisho chako.

7) Lazima uarifu (ujulishe) Huduma ya Hifadhi ya ukimbizi mara moja, kwa haraka kuhusu anwani yako na uwasiliano (namba ya simu), pia na wakati unapo zibadili. Huduma ya Hifadhi ya ukimbizi itatuma kwenye anwani uliyowapa, dokimenti, cheti, inayohusiana na ombi lako.

8) Lazima ufike, uje mwenyewe kwa kuongeza muda wa cheti cha mwombaji hifadhi ya ukimbizi (pinki kadi) watakao kupa, siku ijao (next day) baada ya kumalizika kwake.

9) Lazima ujiwasilishe mwenyewe kwenye Huduma, idara ya mahojiano (interview) kwenye tarehe utakaojadiliwa.

10) Lazima huzingatie muda uliongaliwa kwenye hatua mbali mbali la uchunguzi wa ombi lako.